# Utangulizi Kitabu Cha Mwanzo

## Na Heath Stapleton

www.kanisalakristo.com
chimalaheath@yahoo.com
kountzeheath.vox.com

# KITABU CHA MWANZO


Historia Ya Mwanzo Wa Uumbaji

**Vipindi Sita vya Mgawanyo wa Kitabu cha Mwanzo**

1. Uumbaji mpaka gharika, (sura 1-5)
2. Gharika mpaka Ibrahimu (sura 6-11)
3. Ibrahimu, (sura 12-23)
4. Isaka, (sura 24-26)
5. Yakobo, (sura 27-36)
6. Yoseph, (sura 37-50)

**Wazo Kuu Kwa Kila Mgawanyiko**

1. Uumbaji mpaka gharika, (1-5), Adamu, Kaini na Habeli, Seti, Methuselah.
2. Gharika mpaka kwa Ibrahamu, (6-11), Nuhu, Hamu, Yapheti, Babeli.
3. Ibrahimu, (12-23) Ur, Harani, Hebroni, Luthi, Sara, Ishmaeli, Isaka, Unabii wa Mesia.
4. Isaka, (24-26) Kuzaliwa vizazi vyake- Rebeka, Yakobo na Esau.
5. Yakobo (27-36) Haki ya kuzaliwa, maono ya Bethali, Haruni na Labani, Raheli na Lea na wajakazi wake.




6. Yusufu (37-50) – aliyependwa sana na Yakobo – "mwotaji" – aliyeuzwa utumwani Misri – mke wa Potifa – ndoto ya Farao - Yusufu mtawala wa Misri- Kukutana tena na kaka zake, familia ya Yakobo Gosheni.

**KATIKA MWANZO KUNA VIPINDI VITATU**

1. Uumbaji, 1-3
2. Antediluvian Age – Kipindi kabla na wakati wa Ghalika, 4-5.
3. Kipindi cha MaBaba (Patriarchal Age), 6-50.

## UUMBAJI

1. Mfuatano wa vitu.
2. Siku ya kwanza–mwanga, 1:1-5
3. Siku ya pili–kutenganisha nchi, na anga, 1:5-8
4. Siku ya tatu-nchi kavu na mimea, 1:9-13
5. Siku ya nne–jua na mwezi, 1:14-19
6. Siku ya tano- wanyama wa majini na ndege, 1:20-23
7. Siku ya sita-wanyama wa mwitu, wanyama wafungwao, binadamu, 1:24-31
8. Siku ya saba-mapumziko, 2:1-3

## KIPINDI CHA ANTEDI LUVIAN

1. Kipindi cha Edeni-Kuanzishwa kwa makazi, 2:1-3:24.
    a. Kanuni ya Maadili- sheria-kujaribiwa-dhambi-adhabu, 3.
    b. Kanuni ya kiroho- ahadi ya Mkombozi, 3:15.
2. Vizazi viwili- Kaini na Habeli, 4-5
    a. Vizazi vya Kanani–wana wa ulimwengu, 4:17-24
    b. Vizazi vya Seti-vizazi vya Mesia (Kristo), 4:25-5:32
3. Vizazi vilijiunga, 6:1-6
    a. Udhahifu wa jumla, 6:5-7
4. Gharika, 6:7-9:29
    a. Ulimwengu unaadhibiwa.

## KIPINDI CHA WAZAZI –NUHU HADI YUSUFU

1. Maagano na Nuhu (9:8-17) na Ibrahimu, (15:9-21; 17)
2. Kizazi cha Ulimwengu, 10
3. Kuchaguliwa kwa kizazi cha Shemu kwa ajili ya Masia, 10:21-32; 11:10-32
4. Kizazi cha Ham (10:6-20) na Yapeti (10:2-4)
5. Imaya ya Babeli katika Shimari, 11:1-9
    a. Tofauti zilizoletwa na Mungu-kwa kuleta mchafuko wa lugha au kwa kuchanganya lugha.
6. Uzao wa Shemu, 11:10-32
    a. Kuitwa kwa Ibrahim, 12:1-8
    b. Mtu wa Imani.
    c. Agano la Ibrihamu, 15:9-21; 17
    d. Ibrahamu na Luti, 13-14:16
    e. Ibrahimu na Melikizedeki, 14:17-24
    f. Ibrahimu anaahidiwa urithi, 15:4
    g. Ibrahimu na Ishimaeli, 16
7. Urithi Unaahaidiwa Kwa Isaka, 21
    a. Kumtoa Isaka sadaka, 22:1-19
    b. Ndoa ya Isaka na Rebeka, 24
    c. Kuzaliwa kwa Esau na Yakobo, 25:19-34
        1) Kuuza kwa haki ya urithi, 25:27-34

2) Urithi inaibiwa

8. Yakobo Baba Wa Israeli, 27-35
    a. Yakobo akiwa Betheli, 28:10-22
        1) Marejeo ya Agano.
    b. Yakobo akiwa Mesopotamia, 29-30
        1) Kuzaliwa kwa watoto wa kiume kumi na moja.
    c. Kutenga na Labani, 31
        1) Kushindana na malaika, 32:22-32
    d. Yakobo akiwa Kanaani, 33-35
        1) Kuzaliwa kwa Benjamini.
9. Yusufu Mkombozi wa Israeli, 37-50
    a. Anapelekwa utumwani Misri, 37:12-36
    b. Anapendwa na Potifa, 39
    c. Anafungwa, 40
    d. Kufafanuliwa maana ya ndoto, 41:1-40
    e. Waziri mkuu wa Misri, 41:41-57
    f. Yusufu akiwa Misri.
        1) Njaa kubwa, 42-44
        2) Yusufu anatunza Israeli, 45-47
        3) Israeli katika nchi ya furaha ya Gosheni, 47:1-12
        4) Yakobo anatoa unabii akikaribia kufa, 49
            A. Maisha ya madaye ya makabila.
            B. Yuda kabila la Mesia, 49:8-12
    g. Yusufu anahakikishiwa kurudishwa Kanani, 50:22-26
        1) Kufa kwa Yusufu.

## Mwandishi

1. Musa, – Lk.24:44, Yan. 19-23
2. Alizaliwa Misri, Kut. 2:1-2.
3. Wazazi wake walikuwa watumwa Misri
    a. Baba aliitwa Amroni
    b. Mama aliitwaYakobedi, Kut. 6:20
4. Mdogo wa Haruni na Mariamu.
5. Aliokolewa kutoka kwenye mto na akafanywa mtoto wa binti Farao, Kut. 2:3-10.
    a. Akafundishwa kwa hekima yote ya wa Misri, Mdo.7:22.
6. Alitumia miaka 40 uhamishoni Midiani, Kut. 2:11; 4:26.
7. Alitumia miaka 80 kuwatoa Wayahudi kutoka utumwani, Kut. 12:29-15, 14:1-31.
    a. Alipokea amri za Mungu katika mlima Sinai.
8. Aliwaandikia vitabu vya Mwanzo, Kutoka, Mambo Ya Walawi, Hesabu, Kumbukumbu la Torati, Zaburi sura ya 90, na labda ndiyo yeye aliyeandika kitabu cha Ayubu.
9. Kutokutii kulimwondolea haki ya kuingia nchi ya ahadi.
10. Alikufa na miaka, 120 - akazikwa na Bwana katika nchi ya Moabi, Kum.

34:6-8.

**Kitabu Cha Mwanzo**

1. Kiliandikwa, 1500-1425 K.K.
2. Genesis- "Hapa mwanzo."
3. Vitabu vya mwanzo vitano vinaitwa Torati.
    a. Vitabu vya Torati vinafahamika kuwa 3/5 ya Sheria kufuatana na wakubwa wa dini ya Kiyahudi.
    b. Penteteuch – viliandikwa na Wagiriki.

**Dhamira Ya Kitabu**

1. Kutoa kumbukumbu ya mwanzo na maendeleo ya nchi teule ya Mungu.
2. Kumbukumbu ya Mungu na ulimwengu wote (universe).
3. Kuonyesha Mwanzo wa kujifafanua kwa Mungu kwa wanadamu.
4. Kuonyesha Mungu anavyojihusisha na atakavyojihusisha na mwanadamu.
5. Kuonyesha mwanzo na matokeo ya dhambi.

**Uzito Wa Kitabu Hiki**

1. Kitabu hiki kinajibu maswali ya binadamu.
    a. Ninatoka wapi?
    b. Ulimwengu uko vipi na kwa nini?
    c. Dhambi inatoka wapi na kwa nini?
    d. Mwanzo wa Waebrania na dini yao.
    e. Kitabu kilianza na maisha na kilimaliza na kifo.

**MAHUDHULIO MATATU**

1. Mungu-Muumbaji
2. Kushindwa kwa wanadamu kufikia wokovu wa Mungu.
3. Mwanzilishi wa taifa la Waebrania

**UUMBAJI**

1. Mwanzo 1:1-2:25
   A. Kabla ya siku sita tunajua kulikuweko na vitu vitatu.
      1. Mungu alikuwepo 1:1 yeye anayeongea.
      2. Kulikuwepo na Kristo, Yn. 1:1-4, 14-17.
      3. Kulikuweko na Roho, Mwa. 1:2.
   B. Tunajuaje walikuwepo.
      1. Kwa muda gani?
      2. Milele – walikuwepo milele yote.
   C. Tunajua kwa hakikia Mungu aliumba.
      1. Aliumba mbingu na dunia na ilikuwa haina umbo lolote.
      2. Hakuna umbo, hakuna mwanga na hakuna maisha.
2. Siku Sita Za Uumbaji.
   A. Wengi wanadai siku moja katika uumbaji ni zaidi ya masaa 24. Wanadai siku moja ilikuwa miaka mamilioni.
      1. Tukumbuke Mungu aliumba mimea kabla ya jua.
      2. Je, Mimea inaweza kukaa miaka mamilioni bila jua? Jibu ni rahisi.
   B. Siku ya Kwanza -Mwanzo 1-3-5 mwanga- mwanga wa kawaida – jua baadaye.
   C. Siku ya Pili, 1-6, mbingu
   D. Siku ya Tatu, 8-13, Kugawa maji na nchi kavu na kuumba mimea.
   E. Siku ya Nne, 14-19, Jua, mwezi, nyota-zinatawala majira yetu.
   F. Siku ya Tano, 20-23, Wanyama wamajini na ndege.
   G. Siku ya Sita, 24-31, Wanyama wapoli na binadamu.
      1. Mwa. 2:1-25 inaelezea kwa undani zaidi kuhusu namana gani mwanamme na mwanamke waliumbwaje.
      2. Tuliumbwa katika mfano wa Mungu, mwanaume na mwanamke
   H. Siku ya Saba, Mwa. 2:2, Mungu alipumuzika.

**Kuanguka kwa Mwanadamu**
**Mwa. 3:1-24**
**Uumbaji Mpaka Ghalika**
**Mwa. 1-5**

1. Binadamu ni kiumbe sio muumbaji.
    A. Kwa kusisitiza ni mtumishi anawajibika kwa Mungu
        1. Mapenzi yake, malengo yake yanatakiwa kuwa yetu.
        2. Sisi sio chochote kumuuliza maswali, kumjaribu au kumpima.
        3. Tunadaiwa kwake kwa namna nyingi, lakini Mungu haidaiwi kitu chochote, Zab. 115:3, 135:6.
            a. Wengine wanahitaji kujifunza kwa njia ngumu- Nabukkedereza Danieli 4:35.
        4. Tunachotakiwa kufanya ni – kumshukuru- kumwabudu- kumtii- Za. 100:2-4.
    B. Yeye ndiye anayetuelekeza sisi.
        1. Kama alivyofanya Adamu, Mwa. 2:17 na wengine.
            a. Tunapoelewa mili basi
            b. Tunaelewa Uumbaji wa Mungu.
        2. Unapojenga nyumba – ni nani aliyemtumishi?
            a. Mwandamu ana Bwana – na nyumba ina Bwana.
        3. Mwanadamu anao anawamiliki pia mko, 1;28.
            a. Tumia nguvu hiyo, Mwa. 2 :19-20
    C. Binadamu sio Mungu.
        1. Tunaweza kuwa na "miliki”.
        2. Tuliumbwa kwa mfano wa Mungu na sio kuwa miungu, Mwa. 1:26-27.
            a. Kwa thamani kuu kama – kivuli cha Mungu.

2. Tuliumbwa tuishi kwa utulivu.
    A. Moja kwa moja pamoja na Mungu, Mwa. 1:27, 2:24, Mt. 19:3-9.
        1. Siyo peke yetu, Mwa. 2:18.
    B. Pia aliumba uhusiano wa ndoa.
        1. Aliumba wanadamu ili wazaliane, 1:28, 9:7
        2. Kuzaa kwa wamama siyo adhabu, maumivu ni adhabu, 3:16.
    C. Bustani.
        1. Sheria moja – mwanadamu alidhani yeye ni mfalme- mwanadamu usahau.
            a. Usahau kwamba yeye ni kiumbe nasio muumbaji.
            b. Baada ya hapo kuanguka katika dhambi.
3. Kwa nini mwanadamu alianguka?
    A. Nyoka, (mjanja, mnyama), 3:1.
    B. Mwanamke, (Yak. 1:13-15) alijaribiwa, 1 Tim. 2:11-15.
        1. Dhambi ili mfanya mwanamke kuanguka.
        2. Dhambi ni matokeo ya kisubusho.
        3. Mtu hawezi kufanya dhambi tu peke yake, kunasababu ya mtu kutenda dhambi.

a. Kama Hawa alitenda dhambi, lakini hakufanya tu, alikuwa na msaada. Kitu kikamilifu hakiwezi kuwa kichafu bila msaada.

C. Dhambi sio tu tendo.
1. Ni mtiririko au mfumo.
2. Hawa alimsikiliza nyoka badala ya Mungu, 3:1-5.
3. Awagawa manufaa ya muda, 3:6, ya kuwa na hekima.
4. Akachuma
5. Akala
6. Akampa mumewe.
7. Akala, 3:6
8. Kwa hiyo tunajua dhambi ni mtiririko au mfuno.

D. Dhambi inatokea kwa sababu ya ubinafsi na moyo wa choyo
1. Dhambi ya Adam na Hawa ilikuwa zawadi ya kula.
   a. Kwanza walikuwa tayari kula.
   b. Hawakulazimishwa kuifanya.
   c. Tatizo la dhambi ni kuwa tayari kuifanya, Lk. 6:45, Rum. 6:12.
2. Baada ya kutenda dhambi unyonge unatoka.
   a. Dhambi ilimfanya mtu aone haya.
   b. Na anayefanya dhambi atatumia juhudi yote kuificha, Mwa. 3:7.
      1) Kama waliifanya Adamu na Hawa.
      2) Wakajificha, 3:8.
      3) Wakaanza kulaumiana, Adamu akamlaumu Hawa, Hawa akamlaumu nyoka, 3:12.
   c. Dhambi ni tendo kubwa.
      1) Dhambi moja inapofanywa dhambi nyingine hufuatia ili kuifunika dhambi yakwanza isionekane.

E. Nini kilitokea baada ya dhambi?
1. Mungu hutuonyesha wazi jinsi tulivyo, 3:9.
2. Anakuadhibu,

F. Kuna matokeo mengi ya dhambi.
1. Aibu na woga, 3:7.
2. Unyonge, 3:12.
3. Kulaumiwa na Mungu, 3:14-19.
4. Kwa nyoka, 3:14.
5. Mwanamke, 3:16.
6. Kwa mwanamme, 3:17-19.

G. Kuna shughuli nyingi za ulimwengu zilianza bada ya dhambi.
1. Kulima, 4;2.
2. Umwagaji damu, 4:8.
3. Miji, 4:17.
4. Mitala, 4:19.
5. Muziki, 4:21.
6. Viwanda, 4:22.

ZINGATIA: Vitu hivi vyote ni vya ulimwengu ila kimoja tu kinatoka kwa Mungu na vingine vinatoka kwa Kaini.

H. Kitu kimoja cha kiroho kilitoka baada ya dhambi.
1. Sala kumweka Mungu na binadamu karibu.

I. Kuanguka kwa mwanadamu ni laisi.
1. Hawa alijaribiwa.
2. Alisikia na alisikiliza.
3. Alifikiri aliyoyasikiliza.
4. Alifanya dhambi – akasaidia mwingine kutenda dhambi.
5. Mwanadamu alianguka.

4. Dhambi ilitawala ulimwengu, 4:1-9-9:38.

A. Baada ya dhambi ya Adamu na Hawa ulimwengu ukaendelea kuwa uovu zaidi.
1. Kwanza na Kaini na Habeli.
a. Kaini alimwua Habeli kwa kutoa sadaka nzuri.
b. Hii ilipotokea kukawepo na vizazi viwili.
1) Sethi – kizazi cha Mungu.
2) Kaini – kizazi cha ulimwengu.
c. Tatizo lilikuwa kwamba kizazi cha Sethi kikabadilika na kuwa kama kizazi cha Kaini.

B. Ulimwengu ukazidi kuchafuka.
1. Mungu akachoka kwasababu ya uovu.
2. Angalia kizazi cha Kaini, 4:16-24.
3. Kaini aliendelea kuwa mbaya zaidi.

C. Mtoto wa tatu wa Hawa na Adamu ni Sethi, 25-26.
1. Kizazi cha Mungu.
2. Kizazi ambacho Mungu alipendezwa nacho kwa Muda.
3. Angalia aya ya 26 kwamba walikuwa wanaitwa kwa jina la Mungu .
4. Tena sura ya tano ni kizazi cha Adam kwa Sethi kizazi cha Abraham, kizazi cha Daudi mpaka kizazi cha Kristo.

**Chati (1-A)**

**Adamu-Shemu**

| Jina | Umri Wa Kuzaa Mwana | Baada Ya Wana Kuzaliwa | Jumla Ya Umri | Marejeo (Vifungu) Kitabu Cha Mwanzo. |
|---|---|---|---|---|
| **Adamu** | **130** | **800** | **930** | **5:3-5** |
| **Sethi** | **105** | **807** | **912** | **5:6-8** |
| **Enoshi** | **90** | **815** | **905** | **5:9-11** |
| **Kenani** | **70** | **840** | **910** | **5:12-14** |
| **Mahalaleli** | **65** | **830** | **895** | **5:15-17** |
| **Yaredi** | **162** | **800** | **962** | **5:18-20** |
| **Henoko** | **65** | **300** | **365** | **5:21-24** |
| **Mathusela** | **187** | **782** | **969** | **5:25-27** |
| **Lameki** | **182** | **595** | **777** | **5:28-31** |
| **Nuhu** | **600** | **Mwanzo Wa Gharika** | **950** | **7:11-9:29** |
| **Shemu** | **98** | **Mwisho Wa Gharika** | **600** | **11:10-11** |

**Gharika mpaka Ibrahimu**
**Mwa. 6-11**

1. Uchafu wa Ulimwengu, Mwanzo 6.
   A. Hapa tunasoma udhaidu wa ulimwengu, 6:1-7.
      1. Ndoa mbaya na mengineyo.
      2. Kumbuka kizazi cha Sethi kilikuwa kizazi cha Mungu.
      3. Baada ya ya kizazi hiki kuanguka Mungu alikuwa tayari kuharibu vizazi vyote.
   B. Kuongezeka, 6:11.
      1. Inasemekana kulikuwa na watu wengi siku zile kama siku hizi.
         a. Dunia ilikuwepo kwa miaka 1650.
   C. "Wana wa Mungu," walichanganya na watoto wakike wa wanadamu, 6:2.
      1. Kuna natharia nyingine kwamba "wana wa Mungu" ni akina nani
      2. Kuna mawazo makuu matatu  na Chati 1-2 zinaweza kusaidia.

**Chati 1-B**

| Kitu (Jambo) | Nadharia #1 | Nadharia #2 | Nadharia #3 |
|---|---|---|---|
| *"Wana wa Mungu"* | Malaika Walioanguka | Mkondo wa Mungu Upande wa Sethi | Wafalme katika uko wa kifalme |
| *"Binti za Wanadamu"* | Walio katika hali ya kimwili | Mkondo wa Kaini | Watu wa kawaida |
| *"Dhambi"* | Malaika kuchanganya na watu wa kimwili. | Upande wa Sethi walioa upande wa Kaini | Wafalme walioa wamama wakawaida na walikuwa na mitala. |

**Ushahidi**

| Nadharia #1 | Nadharia #2 | Nadharia #3 |
|---|---|---|
| 1) "Wana wa Mungu", hurejea kwa malaika (Ayu. 1; 28:7; Zab. 29:1; 89:7). | 1) Mkondo mtakatifu ulianza. | 1) Wafalme au watawala mara kwa mara waliejea kuwa kama miungu, Kut. 21:6; 26:8, 9, 28. |
| 2) Labda Yuda 6-7 | 2) Sura ya sita inaonyehsa kuhusishwa na sura ya tano. | 2) Wakati fulani waliitwa wana wa Mungu. |
| 3) Septuagint inasema katika Ayubu 1 "Malaika wa Mungu." | 3) Dhambi - Ni habari za kawaida katika siku zile. | |
| 4) Kristo alifundisha malaika hawaoi.  Lakini Yesu hakusema Haiwezikani. | | |

D. Tunaamini "wana wa Mungu" ni kizazi cha Seti, 4:26.
   1. Kizazi cha Sethi, 4:26.
      a. Ambao waitwa katika jina la Bwana.
   2. Baadae wakichanganya na uovu.
      a. Mungu aliuona uovu ghairi kwa nini alimuumba mwanadamu, 6:5.
      b. Baadae akaamua kuwaua wanadamu, 6:7.

2. Gharika, Mwanzo
   A. Nuhu alipata neema machoni pa Bwana, 6:8, (13:22)
      1. Alikuwa na watoto wa kiume watatu.
         a. Shemu, Hamu na Yapheti.
   B. Mungu alimwambia Nuhu mpango wake wa kuondoa uovu duniani.
   C. Alimwambi akutengeneza safina.
      1. Kwa kutumia mti wa mvinje.
         a. Mikono mia tatu urefu wa safina.
         b. Mikono hamsini upana wake.
         c. Na mikono thelathini kwenda juu.
         d. Dirisha moja.
         e. Mlango moja.
   D. Kujaza wanyama
   E. Angalia chati 1-C kuhusu siku za gharika.

**Chati 1-C**
**Vipindi Kadhaa Vya Gharika**

| TAREHE | ADAI YA SIKU | TUKIO | VIFUNGU - MWA. |
|---|---|---|---|
| SIKU YA 14 MWEZI 2 | WALINGOJA SIKU 7 | WALINGIA | 7:4,10 |
| SIKU YA 17 MWEZI 2 | 40 | MVUA | 7:4-6,11,12 |
| SUKU YA 26 MWEZI 3 | MWISHO WA 40 | MVUA ILIACHA | 7:4,11 |
| SIKU YA 17 MWEZI 7 | MWISHO WA 150 | SAFINA ILITUA JUU YA MLIMA ARARATI | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| SIKU YA 1 MWEZI 10 | WALINGOJA 40 | VILELE VYA MILIMA | 8:5-6 |
| SIKU YA 10 MWEZI 11 | WALINGOJA 7 | KUNGURU AKATUMWA | 8:7 |
| SIKU YA 11 MWEZI 11 | WALINGOJA 7 | NJIWA ALIYETUMWA AKARUDI | 8:8-9 |
| SIKU YA 19 MWEZI 11 | WALINGOJA 7 | NJIWA ALITUMWA AKARUDI NA | 8:10-11 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | JAMI LA MZEITURI | |
| SIKU YA 27 MWEZI 12 | | NJIWA ALITUMWA NA HAKURUDI TENA | 8:12 |
| SIKU YA 27 MWEZI 12 | MWISHO WA 150 | MAJI YALIKAUKA KABISA | 8:3 |
| SIKU YA 1 MWEZI 1 | | KIFUNIKO CHA SAFINA KIKAONDOLEWA | 8:13 |
| SIKU YA 27 MWEZI 2 | | NCHI IKAKAUKA KABISA WAKATOKA KATIKA SAFINA | 8:14-19 |

MWEZI MMOJA NA SAWA NA SIKU 30.
MUDA WOTE WALIKAA KATIKA SAFINA NI MWAKA MMOJA NA SIKU 17.
360 + 17 = SIKU 377

SIKU 7 ZA KUNGOJA + SIKU 150 + SIKU 150 + SIKU 70 = 377

KUJAA KWA MAJI, KUONDOKA KWA MAJI NA DUNIA KUKAUKA.

3. Baada ya Ghalaika,
    A. Nuhu alijenga madhabahu, akatoa sadaka.
        1. Mungu akambariki Nuhu.
    B. Baadaye Mungu akawapa sheria inayohusu kuua (murder),
    C. Mungu akatoa upinde wa mvua, 9-13
        1. Kwamba hataangamiza ulimwengu kwa maji tena.

4. Dhambi iliingia ulimwenguni tena, Mwa. 9.
    A. Nuhu alilewa.
        1. Lakini kwa sababu Ham hakumfunika Nuhu – akaadhibiwa.
        2. Akawa mtumwa wa ndugu zake.
            a. Lakini laana iliwekwa juu ya mtoto wake Kanani,
    B. Watoto wa Nuhu.
        1. Yapeti, 10:1 mtoto mkubwa.
            a. Yapeti alibarikiwa kuwa mzao mkubwa.
        2. Shemu mtoto wapili.
            a. Shemu uzao wa Mungu.
        3. Hamu, mtoto wa mwisho, 9:22, 24.
            a. Mtoto wake alilaniwa, kwa kicheko cha Hamu juu ya Baba yake.
        4. Sura ya 10 soma kuhusu vizazi vyao.
        5. Sura ya 11 tena kuhuzu kizazi cha Shemu.

5. Mnala wa Babeli, Sura ya 11.
   A. Angalia historia ya Babeli.
      1. Tena mwanadamu akasahau kwama yeye ni nani.
      2. Akaanza kujenga miji mikubwa na mnara ili wafikie mbinguni.
      3. Kwa sababu watu wote walikuwa wa moja.
         a. Wana lugha moja ilikuwa laisi kwa kufanya hivi.
      4. Mungu akaona upumbavu wao, 11:9
         a. Mungu akawatawanya ulimwenguni mwote.
         b. Akawafanya wawe na lugha mbambali tofauti.
         c. Hapa labda ndipo tulipopata tofauti ya watu.
            1) Mungu akatutawanya akaatusaidia kuishi katika mazingila yetu ya asili.
   B. Mnara uliitwa Mnara wa Babeli-maana yake ni "mnara wa mchafuko."

6. Tena katika sura ya 11.
   A. Tunaona kizazi cha Shemu .
      1. Hiki ni kizazi cha Mungu .
      2. Kutoka kwa Shemu mpaka kwa Ibrahim.
   B. Nuhu aliyetii alitunzwa.

**Chati ya 1-D na 1-E**

| Jina | Umri wa Kuzaa Mwana | Miaka aliyoishi baada ya Kuzaa Watoto | Jumla ya Miaka | Marejeo (Vifungu) |
|---|---|---|---|---|
| **Shemu** | 98 | Mwisho wa Gharika | 600 | 11:10-11 |
| **Shemu** | 100 | 500 | 600 | 11:10-11 |
| **Arfaksadi** | 35 | 403 | 438 | 11:12-13 |
| **Sela** | 30 | 403 | 433 | 11:14-15 |
| **Eberi** | 34 | 430 | 464 | 11:16-27 |
| **Pelegi** | 30 | 209 | 239 | 11:18-19 |
| **Reu** | 32 | 207 | 239 | 11:20-21 |
| **Serugi** | 30 | 200 | 230 | 11:22-23 |
| **Nahori** | 29 | 119 | 148 | 11:24-25 |
| **Tera** | 70 | 135 | 205 | 11:26-32 |

## Maisha ya Ibrahimu

## Mwanzo 12-23
## 2,166-1,991 K.K.

Sasa tunaingia katika kipindi cha mwisho, kipindi cha mababa. Ibrahimu alikua mhusika wa sura za 12-23. Kabla ya kusoma maisha ya Ibrahimu ni lazima utafute ramani ili ufuate safari zake.

Mwanzo 1-8 zinaeleza habari za miaka 1,650.
Mwanzo 8-11 zinaeleza habari za miaka 420.
Mwanzo 12-51 zinaeleza habari za miaka 430.

1. Baba Ibrahimu.
    - A. Ibrahimu alikuwa mtu wa Mungu.
        1. Mtu wa imani-aliyependwa na Mungu.
        2. Anapitwa mfano wa Imani katika, Ebr.11.
        3. Anaitwa "Rafiki wa Mungu".
2. Wito wa Ibrahimu.
    - A. Alizaliwa Ur.
        1. Karibu na mto wa Epharate.
    - B. Mtoto wa Tela, 11:27, 28.
    - C. Mume wa Sara, 11:29 - Ur.
    - D. Mungu alimwita aache nyumba yake nakwenda asipokujua, 12:1, Ebr. 11:8.
        1. Kuwa Baba wa Taifa kubwa, 12:2-3- Harani.
    - E. Akiwa na miaka 75 alitoka Harani pamoja na Lutu, 12:5.
    - F. Akaenda Shekemu nchi ya Kanani.
        1. Akajenga madhabahu Shekemu, 12:6, 7.
        2. Akajenga hema karibu na Bethali na akajenga madhabahu ya Mungu-Betheli, 12:8.
    - G. Njaa ikampeieka Misiri, 12:10-13.
        1. Sara akepelekwa katika nyumba ya Farao kama dada yake Ibrahim na Farao akapata pigo, 12:14-17.
        2. Ibrahim akaamuriwa na Farao atoke nje ya nchi yake Misiri, 12:18-20.
    - H. Ibrahimu aliacha Misiri na kwenda Betheli.
        1. Luti pia alikuwa na mifugo mingi Betheli, 13:1-5.
        2. Luti akapewa chaguo la kwenda kwenye bonde la Yordani lenye tambarale, 13:6-13.
    - I. Mungu akampa Ibrahim nchi kwa mbegu zake.
        1. Aliende Hebroni na kujenga madhabahu, 13:14-18.
    - J. Vita ya wafalme, 14.
        1. Lutu akafungwa.
        2. Ibrahim akamsaidia akamwokoa Lutu na mali zake na kumrudisha Sodoma.
    - K. Alikutana na Melkezedeki, 14:18.
        1. Mfalme wa Salemu (mst. 18).
        2. Ibrahimu akampa 10% ya mateko aliyepata kutoka vita.
        3. Melkesideki alimbariki Ibrahimu.

L. Agano ikarudiwa kwa Ibrahim akamwambia uzao wake utakuwa Misiri.
M. Kuzaliwa kwa Ishmaeli mtoto wa Hagari,
  1. Mamre, sura ya 16.
N. Agano lilifanywa na Ibrahim.
  1. Ibrahimu alikuwa na miaka 99.
  2. Mungu alibadirisha jina lake pale Mamre, 17:1-14.
  3. Isaka alihaidiwa pale Mamre, 17:15-22.
O. Kutembelewa na wajumbe wa Mungu ambao walimwakikishia Ibrahimu na Sara kupata mtoto katika umuri wa uzeeni, 18:1-16.
P. Maombi ya Ibrahimu kwa Sodoma na Gomora, alikuwa pale Mamre 18:23-33.
  1. Kuaribiwa kwa miji kwenye tambarale kuokoka kwa Luti na kuelekea Soari, 19:15-30.
Q. Ibrahimu akiwa Gerari, adithi yake na Abimeleki,
  1. Adithi ya mke wake, 20:12, 20-21 Gerari.
R. Kuzaliwa kwa Isaka, Ibrahimu (100).
  1. Ebr. 11: 11; Gerari 21:1-8.
  2. Ajiri na Ishmaeli walifukuzwa, Gerari, 21:9-21.
S. Agano la Abraham na Abimeleki, 21:22-34- Beer- Sheba.
T. Kutolewa sadaka kwa Isaka, Ebr. 11:17-19- Moriah, 22:1-14.
U. Mungu anarejea agano lake na Abraham anarudi Beeri-Sheba, 22:15-19.
V. Kifo cha Sara.
  1. Ibrahimu ananunua pango la Makpela (Hebroni) na akamzika Sara, 23:1-20.
W. Ibrahimu anawatuma mtumwa wake Mesopotania kumtafutia mke Isaka, 24.
X. Ibrahimu alikufa na miaka 175.
  1. Na akazikwa na Isaka na Ishmaili pamoja na Sara katika pango la Makapela (Hebroni), Mwa. 25:7-10.
Y. Kwa hiyo Ibrahimu alikuwa na maisha yaliyokamilika.
  1. Alimpenda Mungu na kumfuata.
  2. Mungu alimbariki kwa upendo kwa ajili hiyo.
  3. Akamfanya Baba wa taifa.
  4. Kwa uzao wake mataifa yangebarikiwa.
  5. Ibrahimu alimpenda Mungu na akahesabiwa haki.

**Maisha ya Isaka-Mwanzo 24-26-2066-1886 K.K.**

Kuna habari ndogo kuhusu Isaka kuliko Ibrahimu, Yakobo na Yusufu, 21-26.

1. Maisha yake wakati Baba Ibrahimu alikuwa na uhai.
    - A. Isaka alioa kabla Ibrahimu hajafa.
        1. Ibrahimu alitaka Isaka kuoa mwanamke anayemcha Mungu.
        2. Sio mwanamke wa kimataifa au wa ulimwengu.
        3. Kwa hiyo alimtuma mtumwa wake.
        4. Akamwapisha mtumwa wake kwamba amtafute mwanamke anayemcha Mungu.
        5. Mtumwa alikwenda katika mji wa Nohori.
        6. Akampata Rebeka.
        7. Akamsimulia kuhusu Ibrahimu na Isaka.
        8. Walikubaliana naye kuoana na Isaka.
        9. Kwa hiyo Isaka akaoa akiwa na miaka 40.

2. Maisha yake baada ya kuoa.
    - A. Akapata mapacha.
        1. Wote walikuwa wawe wakubwa juu ya mataifa makubwa.
        2. Lakini mkubwa atatumikia mdogo, 25:23.
    - B. Njaa ilimpeleka Isaka Gerari.
        1. Mungu akafanya upya agano aliyefanya na Ibrahimu, 26:3-5.
        2. Alikuwa Gerari.
        3. Alidanganya kuhusu mke wake akasema ni dada yake.
        4. Walipopata ukweli alitafuta ulinzi.
        5. Utajiri wake ukaongezeka.
        6. Baadaye wakaomba kuondoka.
    - C. Bonde la Gerari.
        1. Akachimba visima.
    - D. Akaenda Beer-Sheba.
        1. Mungu alimtokea, 26:24.
        2. Isaka akajenga madhabahu.
        3. Mfalme aliyeomba aondoke alikuja kufanya mapatano na Isaka.
        4. Mtoto wake wa kwanza Esau (umri 40) - alioa Mhiti, mke wa ulimwengu.

3. Uzee wa Isaka, Mwa. 27.
    - A. Isaka alikuwa mzee.
        1. Yakobo alikuwa ameshepata haki ya uzao wa kwanza kutoka kwa Esau.
        2. Lakini sasa alitakiwa kubarikiwa kutoka kwa Baba yake.
            - a. Akamdanganya.
            - b. Esau alichukia sana.
            - c. Yakobo akawa na wasiwasi wa maisha yake na mama yake akampe ruhusa aenda Harani kuishi na Labani.
    - B. Isaka alikufa akiwa na umri wa miaka 180.

**Maisha ya Yakobo**
**2006-1859**
**Mwanzo 27-36**

Aliishi miaka 147.

1. Yakobo kama wengine (Baba na Babu) alikuwa shupavu na kumuweka Mungu kwanza.
    A. Yakobo alikuwa mwelevu wa kudanganya.
        1. Lakini alimuweka Mungu mbele na wala hakusahau kumtumikia Mungu.
    B. Kama yeye alivyokuwa anadanganya na pia alidanganywa zaidi na Labani.
    C. Alikipata kibari machoni pa Bwana na akabarikiwa naye.
    D. Alikuwa na mapacha mdogo wa Isaka na Rebeka, Beer–Sheba, 25:22-26.
        1. Yakobo alipendwa na Mama, 25:27, 28.
        2. Esau alipendwa na Baba, 25:29- 34.
    E. Yakobo alinunua haki ya uzaliwa wa kwanza kwa Esau, Beer–Sheba, 25:29-34.
        1. Yakobo alimdanganya Baba yake kwa kujifanya Esau nakupata baraka za Esau, 27:1-29.
    F. Alitumwa na Isaka na Rebeka kwenda kupata mke, Beer–Sheba, 28:1-7.

2. Yakobo alianza maisha ya kujitegemea mwenyewe na Mungu.
    A. Alilala usiku Betheli akapata maono ya ngazi na malaika Bwana alirejea baraka za Ibrahimu na Isaka kwake Betheli, 28:10-15.
        1. Yakobo akajenga ukumbusho na akafanya agano na Mungu, Betheli, 28:16-22.
    B. Alikwenda Padanaramu nyumba ya Labani.
        1. Kaka yake mama yake.
        2. Akatumikia miaka saba kwa ajili ya Raheli, 29:1-20.
    C. Mdanganyifu alidanganya na Labani akampa Lea na kumfanaya afanye kazi miaka saba mingine kwa mpendwa wake Raheli, Padam–Aram, 25:29- 30.
    D. Watoto wake wa kiume kumi na moja walizaliwa Padam–Aram, 29:31, 30: 24.
    E. Yakobo akafanya mpango wa kuwa tajiri.
        1. Wakapoteza uelewano na Labani, Padam–Aram, 30:25-43; 31:3-21.
        2. Mungu akamwambia arudi Kanani.
    F. Labani akaja kumteka Yakobo.
        1. Wakafanya agano likafanywa katika mlima Giliedi, 31:22-25.

3. Yakobo anarudi kwenye nchi ya Ahadi, Mwa. 32.
    A. Alituma zawadi kwa kaka yake kwa sababu ya woga.
    B. Akishindana na malaika, usiku mzima pale Penieli.
        1. Jina lake likabadilishwa na kuwa Israeli, 32:30.
    C. Kukutana kwa amani kwa Yakobo na Esau.
    D. Yakobo akakaa Shekemu, Mwa. 33.
        1. Tatizo la binti ya Yakobo.
        2. Kuuawa kwa Hamori na familia yake, Mwa. 34.

E. Mungu alimwambia Yakobo aondoke kwenda Betheli, 35:1-15.
   1. Na hapa akajenge madhabahu.
   2. Na Mungu akaongea naye, Betheli, 35:1-15.
F. Kuondoka Betheli na kumzaa Benjamini mtoto wa kiume 12, 35:16-20.
   1. Raheli akafa na akazikwa karibu na Bethelehem, 35:19.
G. Baba yake alikufa.
   1. Aliondoka kwenda Beer-Sheba kumzika Baba yake.
   2. Alionana na kaka yake Esau, Beer–Sheba 35:21-29.

4. Mtoto mpendwa ni mkombozi wake.
   A. Yakobo anampenda sana Yusufu.
   B. Ndoto ya Yusufu walipokuwa Beer–Sheba, 37:1 11.
   C. Akatuma Yusufu kuonana na ndugu zake.
      1. Kuuzwa kwa Yusufu, 37:21- 35.
   D. Njaa inawepeka ndugu za Yusufu.
      1. Wakaenda Misiri kutoka Beer–Sheba iliwatafuta chakula, Mwa. 42-45.
      2. Yusufu alipata cheo kubwa Misri na aliokoa Yakobo na watu wake 70 kutoka njaa.
      3. Wanapata makazi Gosheni.
         a. Na badai wakua watu wenye nguvu.
   E. Baada ya miaka 17 Misri Yakobo alikufa.
      1. Na wakampelekwa kuzikwa Kanaani.
      2. Alizikwa kwenye kaburi la Makapela, 46:1-50.

**Chati ya 1-F**
**Wana Wa Yakobo**

| Mama | Mwana | Maana ya Jina | Kifungu Juu Ya Kuzaa | Mpangilio wa Baraka | Alama Za Baraka | Vifungu vya Baraka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Lea** | Reubeni | Ona, Mwana | Mwa. 29:32 | 1 | Hakujali | Mwa. 49:34 |
| " | Simeoni | Kusikia | 29:33 | 2 | Kaidi | 49:5-7 |
| " | Lawi | Muungano | 29:34 | 3 | Kaidi | 49:5-7 |
| " | Yuda | Sifa | 29:35 | 4 | Simba | 49:8-12 |
| **Bilha** | Dani | Hukumu | 30:6 | 7 | Nyoka | 49:16-18 |
| " | Naftali | Ushindi | 30:8 | 10 | Ayala | 49:21 |
| **Zifa** | Gadi | Bahati Njema | 30:11 | 8 | | 49:19 |
| " | Asheri | Heri | 30:13 | 9 | Chakula Kingi | 49:20 |
| **Lea** | Isakari | Zawadi | 30:18 | 6 | Punda | 49:14-15 |
| " | Zabuloni | Dumu | 30:20 | 5 | Meli | 49:13 |
| **Raheli** | Yusufu | Aniongeze | 30:34 | 11 | Mwenye Kuzaa | 49:22-26 |
| " | Benyamini | Mwana wa mkono wa kuume | 35;18 | 12 | Mbwa Mwitu | 49:27 |

**Maisha ya Yusufu**
**Mwanzo 37-50**

1. Historia ya Yusufu kabla ya kuenda Misri.
    - A. Yusufu alikuwa mtoto wa 11 wa Yakobo.
        1. Mtoto aliyependwa sana na Yakobo.
        2. Mama yake ni Raheli, Mwa. 30:22-24.
    - B. Yakobo alimpenda sana kuliko watoto wengine na akamtengenezea koti la rangi nyingi, walipokua Beer–Sheba, 37:1-1.
        1. Aliwaambia ndugu zake ndoto zake mbili na wakamchukia zaidi, Beer–Sheba, 37:5-11.
    - C. Yakobo alimtuma Yusufu Dothani kuwaangalia kaka zake.
        1. Wakataka kumua.
        2. Yuda akasema wamuuze.
        3. Wakatumbukiza koti lake kwenye damu.
        4. Wakamuuza kwa Wamedi waliokuwa wanaenda Misri.
        5. Potifa afisa wa Farao akamnunua Yusufu, 37:12- 36.

2. Yusufu kwenye nchi ya Misri, mtumwa wa Potifa.
    - A. Wema wa Joseph ukamfanya Bwana wake Potifa ampende ambaye alimfanya awe mwangalizi wa nyumba yake yote, 39:1- 6.
    - B. Mke wa Potifa akashindwa kumpata kumpata Yusufu, na anamsingizia Yusufu akafungwa, 39:7-23.
    - C. Akawatafsiria ndoto wafungwa wawili na zikawa kama alivyo watafsiri, Mwa. 40.
    - D. Miaka miwili baadaye Farao alikuwa na ndoto mbili zilizomsumbua sana na Yusufu akazifisiri miaka saba ya shiba na miaka saba ya njaa.
        1. Akamwambia Farao afanye nini kuhusu hilo kwa baraza la Farao, Mwa. 40.

3. Yusufu akawa Waziri Mkuu wa Misri.
    - A. Farao akamfanya Yusufu kuwa waziri mkuu.
        1. Alifanya vizuri na kuweka akiba ya chakula kwenye gahal la Misiri, 41:37-57.
    - B. Njaa katika Palestina ilifanya Yakobo atume watoto wake waende Misiri kununua chakula.
        1. Yusufu aliwatambua lakini wao hawakumtambua na hakuwaambia yeye ni nani?
        2. Aliwapa chakula na kuweka fedha zao kwenye mizigo yao baraza la Misiri, Mwa. 42.
    - C. Aliwaagiza kurudi tena na Benjamini.

4. Yusufu akawa Mkombozi wa Israeli.
    - A. Alijitambulisha kwa kaka zake na kuwa fanyia wema na kuwapa makazi, Mwa. 43- 45.
    - B. Yakobo na watu wake walienda kuishi Gosheni.

1. Jumla walikuwa 70.
2. Na wote wakawa watu wa kufanyikiwa sana.

C. Yakobo akambariki Ephrahim na Manase watoto wa Yusufu na kutoa unabii kwa makabila baada ya hapo akafa.

1. Yusufu na kaka zake wakamzika na watu wake katika kaburi la Malapela–Hebroni, 46:1-50:13,

D. Baada ya kifo cha baba yao Yusufu aliishi na kaka zake kwa wema.

1. Aliwaahakishia kwamba Mungu atawapa nchi yao.
2. Aliwaomba pindi atakapokufa wapeleke mifupa yake kwenye nchi yao.

E. Alikufa akiwa na miaka 110, Misiri, Mwa. 50:14- 26.

F. Maisha yake yanalinganishwa sana naya Kristo.

1. Alipendwa zaidi ya ndugu zake.
2. Aliuzwa na ndugu zake.
3. Alifungwa na akawa mnyenyekevu.
4. Akiibwa kanzu yake.
5. Alikuwa na mfungwa mmoja aliyeishi na moja aliyepotea.
6. Yusufu aliibuka bila kuegemea na kwa mtu mkubwa kama Kristo.

<u>Chati 1- G.</u>

Kuteteleka Kiroho Kwa Kipindi Cha Wazazi

| **KIZAZI CHA KWANZA** | **KIZAZI CHA PILI** | **KIZAZI CHA TATU** | **KIZAZI CHA NNE** |
|---|---|---|---|
| IBRAHIMU | ISHMAILI NA ISAKA | ESAU NA YAKOBO | YUSUFU - 11 |
| MTU WA IMANI ALIMWANINI MUNGU RAFIKI WA MUNGU | ISHMAILI HAKUWA MWANA WA AHADI. ISAKAI ALIMWITIA MUNGU, ALIMWAMINI MUNGU. | ESAUI IMANI NDOGO ISIYO YA KIROHO. YAKOBOI MWANZONI ALIKUWA MTU WA KUVU. TANA, BAADAYE AKAWA NA IMANI. | YUSUFUI MTU WA MUNGU. ALIOYESHA IMANI KWA NDUGU ZAKE KATIKA TATIZO KUBWA. |
| ALIMJENGEA MUNGU MADHABAHU, MWA. 12:7-8; 13:4,18; 22:9. | ISAKA: ALIJENGA MADHABABU, MWA. 26:25. | YAKOBOI ALIJENGA MADHABAHU, 33:20; 35:1,3,7. | HAKUJENGA MADHABABU. |